Sekta ya Huduma za Nyumbani Wafanyakazi wa Huduma za Nyumbani Masharti ya COVID-19

Hati hii inatumika kwa sekta ya huduma za nyumbani na ni mahususi kwa wafanyakazi wa huduma za nyumbani. Kwa madhumuni ya hati hii, mfanyakazi wa huduma ya nyumbani ni mfanyakazi yeyote ambaye analipwa na mwajiri mmoja au zaidi na anatoa huduma za nyumbani kwa mtu au nyumba kwenye au kuhusu nyumba binafsi kama mfanyakazi wa huduma za nyumbani. Mfanyakazi wa huduma za nyumbani ni pamoja na wafanyakazi wanaolipwa kwa saa au mwenye mshahara, wanakandarasi wa kujitegemea wanaofanya kazi kibinafsi, wafanyakazi wa kudumu na wa muda, wafanyakazi wa muda mfupi. Mwajiri ni pamoja na shirika la kuajiri, watu binafsi, nyumba, na waajiri (m.f., biashara zinazotoa huduma za moja kwa moja, ikiwemo mashirika ya ajira na majukwaa ya mtandaoni) ambao wanamlipa mfanyakazi wa huduma za nyumbani kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja ili atoe huduma kama mfanyakazi wa huduma za nyumbani. Pale panapokuwa na mwajiri zaidi ya mmoja, masharti yanatumika kwa kila mwajiri/uhusiano wa ajira wa mfanyakazi.

Wafanyakazi wengine wa nyumbani wanalindwa na miongozo tofauti kwa sababu kazi zao hazijabainishwa kuwa muhimu kwa mujibu wa Tangazo la Gavana 20-05. Wafanyakazi wa huduma za nyumbani ni wale ambao, wapo au wanaoshughulikia nyumba binafsi, wanatoa huduma za uangalizi binafsi kwa watu wenye ulemavu wa muda mrefu, au wale walio na maradhi, wazee, au walio hatarini, ili kuwasaidia kufanya “shughuli za maisha ya kila siku”, kama vile kula, kuoga, na kuvaa mavazi. Zaidi ya kusaidia shughuli za maisha ya kila siku, mfanyakazi wa huduma za nyumbani pia anaweza kusaidia katika “shughuli za maisha huru katika maisha ya kila siku”, ambazo zinawasaidia watu kuishi kwa kujitegemea katika jamii. Wafanyakazi wahuduma za nyumbani ni pamoja na, lakini sio tu, wale waliobainishwa na State Department of Health chini RCW 18.88B.

Kazi zinazofanywa na Wafanyakazi wa Huduma za Nyumbani zilichukuliwa kama muhimu kwa mujibu wa Tangazo la Gavana la 20-05 na hivyo huduma nyingi zimebaki kama zilivyo wakati wa janga la COVID-19. Masharti ya afya na usalama yanapaswa kuzingatiwa na waajiri na wafanyakazi wa huduma za nyumbani kama ilivyoelezwa hapo chini.

Kadri ambavyo masharti yoyote hayahusiki *kabisa* kwa waajiri wa mfanyakazi mmoja, haipaswi kufuatwa na mwajiri kama huyu.

Imethibitika kwamba wafanyakazi katika sekta ya huduma za nyumbani watakabiliwa haswa na vikwazo katika uwezo wao wa kukataa kufanya kazi, kupata likizo ya ugonjwa yenye malipo, na kupata mafao ya ukosefu wa ajira. Katika hali zote za ajira, waajiri wanapaswa kuvifahamu vikwazo ambavyo wafanyakazi wao wanaweza kukabiliwa katika kupata kinga ya mfanyakazi.

Mahitaji ya Usalama na Afya

Waajiri wote wa huduma za nyumbani wana wajibu wa pamoja wa kuweka mazingira ya kazi salama na yenye afya kulingana na sheria na kanuni za jimbo na serikali kuu. Aidha, lazima wafuate taratibu zifuatazo za usalama wa mahali husika pa kazi za COVID-19 kama zilivyobainishwa kwenye Tangazo la Gavana la “Safe Start” la 20-25.4, na kwa mujibu Masharti ya Jumla na Mawazo ya Kinga kwa Sehemu za Kazi ya L&I. Washington State Department of Health na Washington State Department of Social and Health Services zimeandaa hati ya muongozo wa usalama kwa wafanyakazi:

- Mapendekezo ya Washington State Department of Health kwa Watoa Huduma za Nyumbani

- Mwongozo wa Jimbo la Washington Department of Social and Health Services Watoa huduma wa Kibinafsi (IPs) katika Kutoa Huduma Salama Wakati wa Mkurupuko wa COVID-19

Mwajiri au Mwajiri mwenza anayefanya shughuli za usimamizi, kama vile Mashirika ya Utunzaji wa nyumba na jimbo la Washington, lazima wafuate masharti ya COVID-19 na miongozo ya kuwalinda wafanyakazi, ikiwemo:

- Kuwaelimisha wafanyakazi katika lugha wanayoielewa vizuri kuhusu virusi vya korona na jinsi ya kuzuia maambukizi na sera ya mwajiri kuhusu COVID-19.
- Kuweka umbali wa futi sita kati ya wafanyakazi na wateja wote katika maingiliano yote kwa kiwango kikubwa iwezekanavyo. Pale ambapo kudumisha umbali wa kutengana hakuwezekani kwa kazi mahususi, hatua nyingine za kujikinga zinaweza kutumika, kama vile kutumia vizuizi, kupunguza wafanyakazi au wateja katika maeneo membamba au ya ndani, na panga muda tofauti wa mapumziko na wafanye kazi kwa zamu.
- Kuwapatia bila malipo na kuwahitaji wafanyakazi kuvaa vifaa vya kujikinga (PPE) kama vile glavu, miwani mikubwa ya kujikinga, kikinga uso na barakoa za usoni kama inavyofaa shuhuli inayofanywa. Rejelea Masharti ya Kitambaa cha Kufunika Uso na Barakoa kwa maelezo zaidi. Wafanyakazi wa nyumbani wanaotoa huduma kwa wateja wenye COVID au wenye dalili wanachukuliwa kama watu walio kwenye hali ya “Hatari Kubwa Sana” na lazima wapewe PPE zinazofaa. Wafanyakazi wahuduma za nyumbani wanaotoa huduma kwa wateja wasioonyesha dalili wanapaswa kuchukuliwa kuwa wapo kundi la “Hatari ya Wastani” na wanapaswa kupewa barakoa za upasuaji, na vilevile PPE za ziada kadri inavyofaa kulingana na hali. Aidha, vitambaa vya kufunika uso lazima vitolewe na waajiri na vivaliwe na kila mfanyakazi asiyefanya kazi peke yake au anapotekeleza majukumu katika jamii isipokuwa kama hali yake ya kuwa hatarini inahitaji kinga ya kiwango cha juu kwa mujibu wa kanuni na mwongozo wa usalama na afya wa Department of Labor & Industries. Vitambaa vya kufunika uso vimeelezwa kwenye mwongozo wa Department of Health. Hali za kipekee kwa masharti ya vitambaa vya kufunika uso zinajumuisha unapofanya kazi peke yako kwenye ofisi, gari, au sehemu ya kazi; ikiwa mtu huyo ni kiziwi au ana matatizo ya kusikia, na anawasilianana mtu ambaye anategemea lugha ya ishara kama vile alama na kujieleza kwa uso, kucheza kwa mdomo kama sehemu ya mawasiliano; ikiwa mtu huyo ana tatizo la kiafya au ana ulemavu ambao haufai mtu kuvaa kitambaa cha kufunika uso; au wakati kazi haina maingiliano ya ana kwa ana.

Mwajiri lazima afuate masharti na miongozo ya COVID-19 ili kuwalinda wafanyakazi ikiwemo vipengee vilivyoorodheshwa hapo chini. Wafanyakazi wa huduma za nyumbani walioajiriwa na mteja binafsi na kulipwa kupitia DSHS kama Mtoa Huduma Binafsi amechaguliwa, amepangiwa na kusimamiwa na mwajiri na mteja. Katika hali hizi, DSHS inatoa mwongozo wa kuzuia maambukizi na kuenea kwa COVID:

- Hakikisha unanawa mikono mara kwa mara na kwa usahihi pamoja na udumishaji wa vifaa vya kutosha. Tumia glavu za kutumika mara moja ambapo ni salama na zinapofaa ili kuzuia maambukizi ya virisi kwenye vifaa au bidhaa zingine ambazo zinashirikiwa.
- Hakikisha unasafisha na kutumia kiua vimelea mara kwa mara kwenye sehemu zinazoguswa sana.
- Wapime wafanyakazi na wateja ishara/dalili za COVID-19 wanapoanza zamu zao. Wafanyakazi wa huduma za nyumbani wanapaswa kukaa nyumbani au kwenda nyumbani mara moja ikiwa wanajisikia au wanaonekana wagonjwa. Weka kizuizi katika maeneo ya ofisi ya mwajiri ambaye hajasajiliwa katika jimbo ambako mfanyakazi anawezekana au aliyethibitishwa kuwa COVID-19 alifanya kazi, aligusa sehemu, n.k. hadi eneo na kifaa kitakaposafishwa na kuuliwa vimelea. Fuata miongozo ya kusafisa iliyowekwa na Centers for Disease Control ili kusafisha sana na kuua vimelea.

- Wajulishe wafanyakazi wa huduma za nyumbani haraka baada ya mwajiri kugundua kwamba inafahamika kwamba kutokana na kazi zao walikaribiana na watu waliothibitika kuwa na maambukizi ya COVID.

Mfanyakazi anaweza kukataa kufanya kazi isiyo salama, ikiwemo hatari zilizoletwa na COVID-19. Mfanyakazi wa huduma za nyumbani ambaye anaamini mazingira yake si salama lazima awasiliane na aidha mfanyakazi wa jamii au msimamizi wa shirika. Ni ukiukwaji wa sheria kwa mujibu wa RCW 49.17 kuchukua hatua zisizofaa dhidi ya mfanyakazi ambaye ameshiriki katika shughuli zinazolinda usalama kwa mujibu wa sheria kama kukataa kwao kwa kazi kunakidhi masharti fulani. Maelezo yanapatikana kwenye machapisho haya: Brosha la Ubaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi na brosha yaKihispania ya Ubaguzi wa Usalama na Afya.
Wafanyakazi ambao wamechagua wenyewe kujiondoa sehemu za kazi kwa sababu wanaamini si salama kufanya kazi kutokana na hatari ya kuambukizwa COVID-19 wanaweza kupata baadhi au mafao ya ukosefu wa ajira. Waajiri lazima watoe chaguo kwa watu walio katika hatari kubwa ambao wanalindwa na Tangazo la 20-46 za kupata likizo iliyogharamiwa na mwajiri au mafao ya ukosefu wa ajira iwapi mpango mbadala wa kazi hauwezikani. Wafanyakazi wengine wanaweza kupata likizo ndefu ya familia na ya matibabu iliyojumuishwa kwenye Sheria ya Kukabiliana na Virusi vya Korona ya Familia Kwanza, mafao ya ukosefu wa ajira, au mapumziko mengine yenye malipo kutegemeana na mazingira. Taarifa ya ziada inapatikana kwenye Nyenzo za Mkurupuko wa Virusi Vipya vya Korona (COVID-19) na Likizo Yenye Malipo kwa Mujibu wa Family Care Act na Families First Coronavirus Response Act ya Washington.

Wafanyakazi wa Huduma za Nyumbani:
Aidha, wafanyakazi lazima:

1. Wakae nyumbani wanapokuwa anaumwa. Wajulishe mwajiri wanaposhukiwa au inapothibitishwa kuwa wameambukizwa COVID.
2. Wamjulishe msimamizi ikiwa kuna mwanafamilia ambaye anaugua COVID-19 nyumbani. Ikiwa mfanyakazi ana mwanafamilia ambaye anaumwa COVID-19, mfanyakazi huyo lazima afuate masharti ya kujitenga/kukaa karantini kama ilivyotolewa na Department of Health ya Jimbo.
3. Kabla ya kufika kazini, piga simu kwanza na uulize ikiwa mtu unayempatia huduma ana dalili kama vile homa, kukohoa au matatizo ya kupumua ambayo ni mapya kwao. Iwapo ni hivyo, zingatia iwapo huduma zinaweza kucheleweshwa au ufuate tahadhali zilizoorodheshwa kwenye hati ya Muongozo wa Huduma za Nyumbani.
4. Dumisha angalau umbali wa futi sita kutoka kwa watu wengine ndani ya nyumba kadri iwezekanavyo. Pale umbali na watu wengine hauwezekani katika shughuli fulani, hatua nyingine za kujikinga zinapaswa kutumika kama vile matumizi ya vitambaa vya kufunika uso na PPE.
5. Nawa mikono mara kwa mara, mwanzo na mwisho wa zamu yako na kabla na baada ya kuandaa chakula au kugusa majimaji ya mwili. Nawa mikono kwa sabuni kwa angalau sekunde 20 au utumie kitakasa mikono kinachojumuisha angalau 60% ya kileo.
6. Epuka kushika sehemu au vifaa ndani ya nyumba kadri iwezekanavyo. Safisha sehemu zinazoguswa mara kwa mara unapofanya kazi.

Mwajiri ambaye ni mtu binafsi anayemwajiri mfanyakazi wa huduma za nyumbani ili kutoa huduma kwenye nyumba kwake mwenyewe:

7. Mjulishe mfanyakazi wa huduma za nyumbani wakati mteja anapokuwa chini ya karantini ya nyumbani, anaanza kuonyesha dalili zinazohusiana na COVID-19.
8. Pale mfanyakazi wa nyumbani anapokuwa au anapoonekana mgonjwa, anatakiwa kutofanya kazi hadi atakapopona.
9. Nawa mikono mara kwa mara pale mfanyakazi wa nyumbani anapokuwa nyumbani.

10. Dumisha umbali wa futi sita kutoka kwa mfanyakazi wa huduma za nyumbani kadri inavyowezekana na upunguze muda unaoutumia kukaa karibu na mfanyakazi wa huduma za nyumbani.

Miongozo ya mahali pa kazi

11. Mtu yeyote ambaye yupo kazini na anaweza kuvaa barakoa wakati huduma ya uangalizi wa nyumba inatolewa anapaswa avae angalau kitambaa cha kufunika uso ili kuzuia hatari ya maambukizi katika jamii. Watu kama hao pia wanahimizwa sana kufuata masharti yote ya PPE. Pale inapowezekana, watu waliopo kwenye nyumba wakati mfanyakazi wa nyumbani anafanya kazi wanapaswa kukaa mbali ya mfanyakazi wa nyumbani na kutoka kwenye vyumba vidogo kwenda kwenye vyumba vikubwa ili kudumisha umbali kati yao na mfanyakazi huyo wa nyumbani. Watu walio mahali pa kazi wanaweza kushindwa kutii, na hawapaswi kutii uvaaji wa kitambaa za kufunika uso na/au PPE kutokana na ulemavu wa utambuzi, ulemavu wa viungo au ukuaji.
12. Punguza muda wa maingiliano Ikiwa huwezi kujadili mambo muhimu kwa njia pepe, punguza muda wa maingiliano ya ana kwa ana na udumishe umbali wa futi sita wakati wote wa mazungumzo yoyote. Watu ambao wanapata huduma za nyumbani wanaweza kushindwa kutii, na hawapaswi kutii, masharti ya umbali na muda kwa sababu ya ulemavu wa utambuzi, viungo au ukuaji.
13. Karatasi ya shashi na mapipa ya taka lazima yawepo mahali pa kazi au nyumbani.
14. Waajiri watawajulisha wafanyakazi kuhusu haki zao za kujiondoa wenyewe kwenye mahali pa kazi kama hawaamini kuwa ni salama, vilevile uwezekano wa kupata likizo au mafao ya ukosefu wa ajira kutokana na hali hiyo.
15. Ikiwa mfanyakazi wa nyumbani anatarajiwa kufanya kazi ya ziada, kama vile usafishaji na uuaji vimelea, hili linapaswa kujumuishwa kwenye makubaliano ya maandishi na wafanyakazi lazima wafidiwe kwa muda waliofanya kazi.
16. Mafunzo yote ya wafanyakazi wa kituo cha kazi lazima yafanyike katika muda wa saa rasmi za kazi.
17. Wakati inawezekana wafanyakazi watarajiwa kufasiri katika gari tofauti wakielekea mahali pa kazi, mtu mmoja kwa gari moja.
18. Ikiwa wafanyakazi wanakutana sehemu ya katikati na kusafiri kwenda mahali pa kazi kwa gari linalomilikiwa na kampuni, toa gari moja kwa kundi moja la wafanyakazi na usibadilishe. Kusafiri kwenye gari linalomilikiwa na kampuni au gari jingine la watu wengi litapunguzwa idadi kwa 50% ya uwezo wa gari na kufuata masharti ya umbali wa mtu na PPE kama ilivyoelezwa kwenye Masharti ya Kitambaa cha Kufunika Uso na Barakoa.

Pale inapowezekana, mambo yanayohusu usalama na afya ya mfanyakazi inategemea hatua ya utekelezaji chini ya L&I's Division of Occupational Safety and Health (DOSH).

- Waajiri wanaweza kuomba ushauri na usaidizi wa kujikinga kutoka kwa L&I's Division of Occupational Safety and Health (DOSH).
- Malalamiko ya usalama na afya mahali pa kazi yanaweza kuwasilishwa kwenye Kituo cha Simu za Usalama cha L&I DOSH: (1-800-423-7233) au kwa barua pepe kwenda adag235@lni.wa.gov.
- Maswali ya jumla kuhusu jinsi ya kutii desturi za makubaliano yanaweza kuwasilishwa Business Response Center ya jimbo kwenye https://coronavirus.wa.gov/how-you-can-help/covid-19-business-and-worker-inquiries.
- Ukiukaji mwingine wote unaohusiana na Tangazo la 20-25 unaweza kuwasilishwa kwenye https://bit.ly/covid-compliance.